# Mdhihiriko wa Kionjo cha Usangwini kwa Mhusika Willy Gamba katika Riwaya ya *Njama*

Athumani S. Ponera
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere
&
Gervas A. Kasiga
Chuo Kikuu cha Dodoma

**Ikisiri**

Maudhui ya kazi za kifasihi hufika kwa hadhira kupitia wahusika. Watunzi huwajenga wahusika hao kwa kutumia mbinu mbalimbali huku wakiwavisha haiba na mujukumu ambayo, aghalabu, huendana na vionjo maalumu vya haiba (*psychological temperaments*). Shabaha ya makala hii ni kufafanua namna ambavyo sifa na majukumu ya mhusika wa kazi za kifasihi huendana na vionjo vya kihaiba anavyojengwa navyo. Ufafanuzi wetu unaegemezwa kwenye uhusika wa Willy Gamba katika riwaya ya *Njama*. Tunaonesha namna anavyotekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na sifa za kionjo cha usangwini ambacho ni mojawapo ya vionjo vikuu vinne vya kihaiba.

## 1.0 Utangulizi

Kazi nyingi za kibunilizi zimekuwa zikiongozwa na wahusika. Wahusika ni binadamu au viumbe wasio binadamu wanaotumiwa na mtunzi kuwasilisha yale anayoyakusudia kwa hadhira yake (Njogu na Chimerah, 2011; Mulokozi, 2017). Mhusika wa kazi ya kibunilizi hujengwa na hisia maumbo, matendo, matarajio, morali, na haiba ambayo huwa na dhima ya kuburudisha au kutoa mafunzo fulani kwa hadhira ya kazi husika. Wahusika huweza kuainishwa kwa kutumia vigezo kama vile maumbile, dhima au mchango wao (kiasi cha ujitokezaji), pamoja na muundo (uhusiano wa mhusika mmoja na wenzake). Kupitia vigezo hivi, tunapata aina za wahusika kwa kutumia istilahi kama vile mhusika mkuu, mhusika bapa, mhusika shinda, mhusika kivuli na mhusika halisi. Istilahi nyingine zinazohusiana na uainishaji wa wahusika ni mhusika mkwezwa, mhusika wa kimapinduzi, mhusika wa kidhanaishi, mhusika wa kisaikolojia, mhusika kaida na mhusika jumui (Mlacha na Madumulla, 1995; Madumulla, 2009; Njogu na Chimerah, 2011; Mulokozi, 2017). Kwa kuwa shabaha ya makala hii si kuainisha wahusika, tunaishia kudokeza tu kwa jumla.

Mhusika akijengwa, hubebeshwa pia sifa za kionjo cha kihaiba kimoja au zaidi. Waandishi, kwa kujua au kutokujua, wamekuwa wakiwajenga wahusika wao kihaiba na kimatendo katika namna inayoendana na vionjo vya kihaiba. Ni maoni

yetu kuwa jambo hili (uhusiano kati ya haiba na matendo ya mhusika katika kazi ya kibunilizi) halijashughulikiwa katika ufafanuzi wa kitahakiki au kitafiti. Kwa hiyo basi, makala hii inafafanua uhusiano wa haiba na uhusika wa mhusika mmoja tu—Willy Gamba—ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Njama*. Tunaonesha namna anavyotekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na sifa za kionjo cha usangwini ambacho ni mojawapo ya vionjo vikuu vinne vya kihaiba kama tulivyoeleza hapo chini.

## 2.0 Vionjo vya Kihaiba na Matumizi yake katika Bunilizi

Vionjo vya kihaiba ni dhana yenye mwegamo wa kisaikolojia (elimu ya akili) na kifiziolojia (elimu ya viungo vya mwili). Martin & Bobgan (1992) na Aras (2015) wanamtaja Hippocrates ambaye ni mwanasayansi wa Kiyunani kuwa ni miongoni mwa wataalamu wa mwanzo kutambulisha dhana hii ya vionjo vya kihaiba kupitia taaluma za saikolojia na fiziolojia. Dhana ya 'kionjo' katika makala hii tunaitumia kumaanisha asili ya tabia au hali ya mtu aliyozaliwa nayo. Kwa hiyo, vionjo huhusu upekee wa mwonekano wa mtu kitabia na kimatendo. Dhana ya 'haiba' humaanisha jumla ya mwonekano wa mtu kimwili, kimaono, kisaikolojia, kiakili, na kijamii. Haiba ya mtu ni matokeo ya vionjo vya kuzaliwa navyo pamoja na athari za kimazingira au makuzi (Aras, 2015; Okal, Ambuyo, & Amukowa, 2012).

Hali hiyo ya upekee wa mwonekano au mwenendo wa mtu hutokana na uwiano wa viambato vinavyopatikana katika vimiminika vilivyomo katika mwili wa mwanadamu. Kwa mujibu wa Septiana (2017) na Ekstrand (h.t.), viambato hivyo hupatikana katika vimiminika muhimu vinne ambavyo ni: maji (*phlegm*)[1], damu (*haima*), nyongo nyeusi (*melaina chole*) na nyongo ya njano (*xanthe chole*). Kuzidi kwa kimiminika kimojawapo katika mwili wa mwanadamu husababisha kuwapo kwa kionjo fulani kinachojenga upekee wa kihaiba kwa mtu huyo. Vionjo hivyo vipo vinne vikiakisi vimiminika vinne vilivyotajwa. Navyo ni: Uflegmatiki (*Phlegmatic*), Usangwini (*Sanguine*), Umelankoliki (*Melancholic*) na Ukoreliki (*Choleric*) (Martin & Bobgan 1992; Aras, 2015; Okal, Ambuyo, & Amukowa, 2012; Septiana, 2017; Ekstrand, h.t). Kwa mujibu wa Ekstrand (h.t: 1), hakuna mwanadamu mwenye aina moja tu ya kiambato kati ya hivi vinne, bali kila mwanadamu ana kiasi fulani cha viambato hivi katika vimiminika vyake. Kwa hiyo, kinachowatofautisha watu kihaiba ni aina ya kiambato kinachozidi kuliko vingine. Hii ni kwa sababu kila kionjo kina upekee wake wa kitabia. Anaongezea kuwa, kila jambo ambalo mwanadamu hufanya huongozwa na sababu fulani. Sababu anazozirejelea hapa ni hivi vionjo.

Hapa tunatoa maelezo mafupi ya vionjo vya kihaiba visababishavyo upekee kwa kila mwanadamu anapotenda na kuamua mambo ndani ya maisha yake. Kionjo cha kwanza ni cha Uflegmatiki. Kionjo hiki hujengwa na uwingi wa kiambato cha *phlegm* kinachopatikana kwenye maji yaliyomo ndani ya mwili.

[1] Istilahi hii na nyingine zilizo katika mabano katika aya hii chimbuko lake ni lugha ya Kigiriki.

Watu wenye kionjo hiki ni wandani (wasiri); yaani huwa si wawazi katika kuelezea mambo au hisia zinazowagusa. Aidha, huwa wapole, wenye kuaminika, wenye uwezo mkubwa wa kuwaza, hujidhibiti na kudhibitika kirahisi, wapenda amani (wasio na rabsha), na wepesi kuongozeka (Media Sportlight, 1994).

Kionjo cha pili cha kihaiba ni cha Umelankoliki. Watu wenye kionjo hiki cha kihaiba huwa na uwingi wa kiambato cha *melaina chole* kinachopatikana kwenye nyongo nyeusi iliyomo miilini mwao. Kisaikolojia, watu hawa ni wandani wasiopenda kuchangamana na watu wengine katika jamii. Ni vigumu kujua ni hisia gani walizonazo katika kipindi fulani. Hutenda mambo yao kwa ukamilifu mkubwa na namna bora. Licha ya kutenda mambo katika namna bora, bado huwa watu wasioamini katika matarajio ya unyoofu wa mambo. Huwa ving'ang'anizi wa mambo na wasiokubali mabadiliko. Daima hufanya mambo wakiwa na matarajio makubwa. Tabia hizi huwafanya wawe wagunduzi wa kisayansi au kuwa wabunifu mahiri wa kisanaa (Martin & Bobgan, 1992).

Kionjo cha tatu cha kihaiba ni cha Ukoleriki. Watu wenye kionjo hiki cha kihaiba huwa na uwingi wa kiambato cha *xanthe chole* kinachopatikana kwenye nyongo ya njano iliyomo miilini mwao. Sifa kubwa ya watu wenye kionjo hiki cha kihaiba ni kuwa wawazi sana na hisia zao huonekana wazi kulingana na matendo wanayoyafanya katika jamii. Sifa nyingine ni kupenda kujitokeza au kujichomoza popote wawapo ili wajulikane, huwa na tamaa ya kuwaongoza wengine na kuwa vinara katika kila jambo na ni rahisi kwao kuumia kihisia pindi wanaposhindwa kuyafikia matamanio yao. Zaidi ya hizo, huwa ni wakorofi na wenye kutumia mabavu, na wakati mwingine, hufanya mambo bila ya kutumia fikra ili tu wayafikie malengo yao.

Kionjo cha nne cha kihaiba ni cha Usangwini. Watu wenye kionjo hiki huwa na uwingi wa kiambato cha *haima* kinachopatikana kwenye damu. Kiambato hiki huwa na kiasi kikubwa cha hewa. Kuwapo kwa kiasi kikubwa cha hewa katika damu huifanya miili yao kuwa na msisimko mkubwa, ambao hatimaye, huwafanywa wawe na hali ya uchangamfu wa kiwango cha juu. Hiki ndicho kinachofafanuliwa katika makala hii. Vionjo vingine vitatu havitatazamwa katika ufafanuzi kwa sababu ya mipaka ya makala. Kwa kuwa kionjo hiki cha kihaiba ni mhimili wa makala hii, tutaeleza sifa zake kwa kirefu kidogo. Kwa kiasi kikubwa, watu wenye kionjo hiki cha haiba huwa na sifa zifuatazo:

a) Ni wasondani (huwa na tabia ya kutoficha mambo, hisia au tabia zao [husema waziwazi]);
b) Huwa wepesi kusomeka kihulka kwa sababu ni watu wasioficha hisia zao katika jamii inayowazunguka;
c) Huwa na kipaji kikubwa cha uongeaji;
d) Hupenda kusaka marafiki wapya (huwa wepesi kutengeneza marafiki);
e) Ni wacheshi na wenye shauku ya kufanya mambo mbalimbali;
f) Huwa na kipaji cha kupendwa na hupenda kujichanganya kwenye mikusanyiko;

g) Huwa wenye busara pamoja na akili nyepesi na ya kibunifu katika kung'amua au kutatua mambo;
h) Hupenda kujiweka katika hali ya mvuto wa kimwili (hujiweka katika utanashati au urembo ili kuwavutia wengine);
i) Hupenda hali ya ufutuhi (kama vile dhihaka, mafumbo, kejeli);
j) Huwa na uthubutu, hawana haya katika kufanya jambo lolote;
k) Hujiamini (hawana hofu), na hawakati tamaa;
l) Huwa na upendo na huruma kwa wengine;
m) Ni watu wasio na majivuno katika mambo wanayoyatenda na kufanikisha;
n) Wakati fulani hupenda kuwa peke yao wakitafakari; na
o) Ni nadra kuwa na hasira za ghafla (Aras, 2015; Ekstrand, h.t.).

Vionjo hivi vinne vya kihaiba tulivyovidokeza hapo juu hujitokeza, hutumika na huathiri vipengele vingi vya maisha ya mwanadamu kama vile siasa, uchumi, mahusiano ya kijamii, uongozi, utabibu, teolojia na malezi (Okal, Ambuyo & Amukowa, 2012). Katika fasihi, vionjo vya kihaiba hujitokeza katika uundaji wa wahusika kwa kurejelea tabia na majukumu wanayopewa na watunzi ili kuwasilisha mawazo yanayolengwa katika bunilizi husika. Kisaikolojia, matendo, tabia na maamuzi wanayoyachukua wahusika waliopo ndani ya kazi ya kibunilizi huenda sanjari na namna walivyojengwa katika kuyabeba na kuyatenda mambo hayo. Kufanana au kuendana kwa ujenzi wa tabia na matendo au tabia za wahusika hutokana na mantiki na ithibati inayodhihirika kadiri bunilizi inavyosonga mbele. Mantiki na ithibati hizo, hatimaye, husababisha hadhira ya kazi ya kifasihi kuuamini uhusika wa mhusika fulani pindi mhusika huyo anapoonesha tabia au matendo kama vile ya kukarahisha, kufurahisha na kusikitisha. Kwa jicho la kisaikolojia, chambilecho Ekstrand (h.t.), yote ambayo mtu (kwa muktadha wa makala hii ni mhusika) anayafanya husukumwa na kionjo maalumu cha kihaiba alichonacho.

Hivyo basi, katika kuangazia mwingiliano huo kati ya uhusika wa wahusika katika kazi za kifasihi na vionjo vya kihaiba, tunatumia kionjo cha Usangwini. Tunafafanua jinsi Usangwini unavyojitokeza katika kumuunda mhusika Willy Gamba katika riwaya ya *Njama*. Tunataraji kuwa ufafanuzi huo utatoa msaada mpana katika kuakisi uhalisi wa hulka zinazounda wanajamii pamoja na tabia au matendo yao. Vilevile, utawasaidia watunzi wa bunilizi kujenga wahusika wanaofanikisha uwasilishaji wa maudhui yanayohusu mabadiliko ya kitabia kwa wanajamii.

## 3.0 Muhtasari wa Riwaya ya *Njama*

*Njama* ni mojawapo ya riwaya zilizotungwa na Aristablus Elvis Musiba. Riwaya nyingine za mwandishi huyu ni *Hofu*, *Kikosi cha Kisasi*, *Uchu*, *Hujuma*, *Kivuli*, *Kufa na Kupona* na *Kikomo*. Toleo linaloshughulikiwa katika makala hii lilichapishwa mwaka 1981 na Continental Publishers. Hii ni miongoni mwa riwaya pendwa za Kiswahili. Riwaya hii inabeba sifa zote za msingi za riwaya pendwa.

Miongoni mwazo, chambilecho Madumulla (2009), ni ya maudhui yake kufunikwa na fani. Riwaya ya *Njama* imejengwa katika namna inayohitaji msomaji wake awe makini ili kuvuna maudhui. Vinginevyo, anaweza kuishia kumezwa na mbinu za kipelelezi na za kimapigano zinazooneshwa na wahusika wake. Kwa kigezo cha usimulizi, riwaya hii inawekwa katika kundi la riwaya za kimonolojia. Hii ni kwa sababu kwa kiwango kikubwa imesimuliwa kwa kuegemezwa kwenye nafsi ya kwanza umoja. Kwa hiyo, mtunzi amemtwisha mhusika wake mkuu, Willy Gamba, jukumu la kusimulia vitushi vyote vya riwaya hii. Mbali na Willy Gamba ambaye ni mhusika mkuu, mtunzi amewatumia wahusika wengine wengi. Amewagawa wahusika hao katika makundi makubwa mawili, la wawi na wema. Miongoni mwa wahusika wa kundi la wawi ni Chimalamo, Shuta, Sikazwe na Max. Kundi la wema lina wahusika kama vile Willy Gamba, Veronika Amadu, Sherrif Amadi, Zabibu Abeid, Eddy na Chifu. Mtunzi ameiegemeza riwaya hii kwenye mapambano baina ya makundi haya mawili ya wahusika. Mapambano hayo yamekitwa katika kisa cha kupeleleza upotevu wa silaha za kisasa zilizotarajiwa kutumika katika kuendeleza harakati za ukombozi wa nchi za Kiafrika, hususani Kusini mwa Afrika, ambazo zilikuwa chini ya mazonge ya kutawaliwa na mabeberu. Licha ya maudhui yanayohusu upotevu wa silaha hizo, riwaya pia imesheheni epistemolojia kuhusu masuala ya kisiasa yaliyokuwa yanajiri ulimwenguni mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980. Mathalani, msomaji anamulikiwa hali ya kisiasa iliyokuwapo ulimwenguni wakati huo, ndani na nje ya bara la Afrika. Zaidi, riwaya imebeba tunu muhimu za kihistoria na kiutamaduni.

## 4.0 Wasifu wa Mhusika Willy Gamba

Willy Gamba ni mhusika anayejitokeza kwa kujirudiarudia katika riwaya za Aristablus Elvis Musiba tulizozitaja hapo juu. Katika kazi hizo zote mhusika huyu anapewa uongozi katika kupeleleza, kutanzua vitanzi vya maswali na mafumbo magumu yanayohusiana na visa mbalimbali, kupanga mashambulizi pamoja na mapigano. Kiwajihi, Willy Gamba anajengwa katika kazi hizo kuwa na miaka takribani thelathini. Ni kijana mtanashati anayewavutia wasichana na wavulana kwa urafiki wa mapenzi au urafiki wa kawaida, mtawalia. Pia, ni kijana mwenye kiwango kikubwa cha hisa ya akili (*Intelligence Quotient)*. Sifa hii ya kuwa na kiasi kikubwa cha hisa ya akili ndiyo kiungo muhimu cha kubebeshwa hizo sifa nyingine. Mathalani, kutokana na sifa hii tunaoneshwa jinsi Willy Gamba alivyo mwepesi wa kufikiri na kujenga hoja maridhawa katika mijadala, kufikiria njia za kujinasua pale anapokuwa katika hali ngumu dhidi ya adui, pamoja na kuunganishaunganisha mambo madogomadogo ili kupata jambo kubwa na muhimu katika kuelekea kwenye jawabu la fumbo fulani. Vilevile, Willy Gamba amejengwa kama mhusika mwenye mbinu zisizoshindwa katika mitindo mbalimbali ya mapigano, ama ya kutumia silaha au viungo vya mwili.

**5.0 Ufafanuzi wa Sifa za Usangwini katika Uhusika wa Willy Gamba**

Tumedokeza hapo juu kuwa, ili uhusika wa mhusika yeyote wa kazi ya kifasihi ulete athari kwa hadhira, ni lazima fanani ausuke kwa kuwianisha na vionjo fulani vya kihaiba. Hivyo, katika sehemu hii tunadondoa baadhi ya 'matukio' yaliyomo katika riwaya hii teule ili kuthibitisha namna kionjo cha kihaiba cha Willy Gamba kinavyohusiana na majukumu anayoyatekeleza riwayani. Tunadondoa baadhi tu ya matukio hayo tukitarajia kuwa yatatoa uwakilishi unaotosha kutoa picha ya jumla ya sifa za usangwini. Dhana ya 'matukio' tunaitumia katika makala hii kumaanisha kipande cha matini kinachodokeza kitendo au tabia tunayoikusudia. Matukio yenyewe ni haya:

Tukio la kwanza linalotudokezea usangwini wa mhusika Willy Gamba ni hili:

> Ndege hii iliyokuwa ikielekea Freetown, ilikuwa tayari kuendelea na safari yetu. Mimi ndiye nilikuwa abiria wa mwisho kuingia ndani ya ndege maana mambo ya kujitangulizatanguliza mbele, rafiki yangu, mara nyingi yanaweza kukuletea kidamasi. Nilipoingia nilianza kuangaza mahali pa kukaa maana vilevile lazima unaposafiri usikae na watu wa ovyoovyo tu kwani wengine wana mikosi. Kama wewe hujui namna ya kuwatambua watu wenye mikosi basi nitafute siku moja nitakunong'oneza (uk. 8).

Haya ni maneno ya mhusika Willy Gamba. Jambo linalobainika katika tukio hili ni tabia yake ya usondani katika kuelezea fikra au hisia zake. Mara nyingine, katika kuonesha uwazi wake wa kihisia, msangwini huyu anatumia maneno yenye kukirihisha na yanayojenga taswira ya kufurahisha. Katika ukurasa huohuo wa 8 mwandishi anatuonesha usangwini wa mhusika huyu kupitia sifa ya ucheshi, ukware na usakaji wa marafiki wapya. Willy Gamba anasema:

> Unajua, binadamu wanafahamiana kwa kukutana! Wengine wanafahamiana kwa kukutana mashuleni, kazini, kwenye starehe na wengine safarini kama hivi na kadhalika. Kwa hiyo, binti, mimi ningeonelea vizuri kama tungefahamiana (uk. 8).

Hapa alikuwa anaongea na msafiri mwenzake ambaye baadaye anakuja kutambulishwa kuwa ni Veronika Amadu. Katika harakati za kuendelea kumzoea binti huyo, mwandishi wa riwaya hii anamsawiri mhusika wake mkuu akitumia 'silaha' ya mvuto wake wa kimaumbile. Tunaelezwa hivi:

> Nilimuonesha tabasamu la kumlainisha. Hili tabasamu huwa nimeliweka kwa wakati huu tu, na huwa silitoi ovyo ovyo. Na kama nilivyotegemea, lilimlainisha. Nakuambia mimi nilizaliwa na bahati ya kuelewana na hawa watoto wa kike, maana ni mara chache sana kunichenga; sijui wewe mwenzangu vipi? (uk. 9).

Mhusika hapa amesawiriwa akiwa na tabasamu lenye uwezo wa kuwavutia wasichana na wanawake kimapenzi. Hii ni sehemu ya sifa walizonazo masangwini wengi katika jamii tunayoishi; yaani ama hujiweka katika hali inayoleta mvuto au hutumia kipengele chochote cha kimaumbile kama silaha ya kujiweka karibu na watu (kwa ajili ya urafiki wa kawaida au ukware).

Mtunzi anazidi kumsawiri mhusika wake huyu wa kisangwini kuwa ni mtu mwenye kupendwa na kupendeka kirahisi na watu, hususani wasichana warembo. Katika ukurasa wa 129, mrembo mwingine, Zabibu Abeid, anaonekana kunaswa kiulaini na mwonekano wa Willy Gamba. Mtunzi anawasilisha hili kupitia maneno yafuatayo ya Zabibu: "Niko tayari kukusaidia; kwanza, kwa sababu umeniokoa, pili kwa sababu unapeleleza kifo cha mpenzi wangu; na, tatu kwa sababu wewe ni kijana mwenye kupendeka". Zaidi, tunaoneshwa hali kama hiyo katika hitimisho la maongezi kati ya Zabibu na Willy Gamba. Mhusika mkuu anatusimulia hivi:

> "Lakini jihadhari... sitapenda kusikia umeuawa, nikisikia tu na mimi nitajiua". Alisema Zabibu akionyesha hali ya mapenzi kana kwamba tumekuwa marafiki siku nyingi. Mimi huwa sielewi kwa nini binadamu hawa hutokea kunipenda mara tu nioneshapo uso wangu (uk. 135).

Tabia ya kisangwini pia tunaiona katika tukio linalohusisha mazungumzo baina ya Veronika Amadu na Willy Gamba. Tukio lenyewe ni hili:

> Nakwambia mtu mara akishakuwa mwandishi basi siku zote yu mwandishi. Msichana huyu alikuwa ananitoa jasho kwa maswali, lakini mimi Willy mambo kama haya ninayapenda maana yananipanua mawazo, hivyo nilimjibu (uk. 14).

Msomaji wa riwaya hii anapofuatilia mfululizo wa mazungumzo ya vijana hawa, anaweza kubaini jinsi Willy Gamba alivyotolewa jasho na maswali motomoto yenye mitego. Hata hivyo, kama walivyo masangwini wengine, Willy Gamba hakukubali kushindwa.

Pia, mhusika mkuu huyu anatuonesha sifa ya usangwini kupitia maongezi yake ya kifutuhi kupitia vipengele kama vile mafumbo, kejeli, na ubeuzi. Ufuatao ni mfano mmojawapo wa maongezi hayo ya kifutuhi:

> "Samahani sana kwa kukuweka ukisubiri." Veronika alitoa udhuru.
> "Kwa Mwafrika, mmewahi sana." Nilimjibu.
> Wote tukacheka (uk. 19).

Hapa alikuwa anamdhihaki Veronika kwa namna laini kutoka na kuchelewa kwake. Dhihaka hiyo ikasababisha kicheko kama tunavyoambiwa.

Sifa zinazohusiana na masuala ya urembo, utanashati na mvuto kwa mhusika sangwini au marafiki zake inajitokeza tena wakati mtunzi anapotuaridhia wajihi wa Hadija, mchumba wa Sherriff. Tumedokeza awali kuwa msangwini hupenda kujiweka katika hali ya mvuto wa kimwili (ili kuwavutia wengine). Willy Gamba (Msangwini) anatuambia hivi kuhusu Khadija:

> Yaani si kwamba alikuwa mzuri sana wa sura ila tu macho yake na umbo lake lilileta msisimko wa pekee kwa mwanaume. Sijui kama wewe nawe umewahi kuona msichana wa aina hii? Kama hujawahi, bahati yako mbaya. Tafadhali fanya kila njia usafiri uone mengi. Kwa hiyo, Khadija alikuwa na uzuri wa kufaa. Kwa sura na umbo lake, Sherriff alikuwa amejipatia mchumba mrembo (uk. 19).

Hizi ndizo sifa za watu wanaohusiana na kuamiliana na mhusika wa kisangwini. Khadija ambaye sifa zake zimetongolewa katika tukio hili ni mchumba wa Sherriff. Sherriff ni mshirika (au komredi, kama aitavyo mwandishi mwenyewe katika uk. 61) wa Willy Gamba; kwa hiyo, 'ndege wa rangi moja huruka pamoja'! Hali ya kuendana huko kwa wahusika wanaoamiliana na Willy Gamba inaendelea kuelezwa katika tukio hili:

> Tulirudi hapo mezani, tukiwapitia wasichana wetu, tukaondoka na kuwasindikiza akina Sherriff mpaka kwenye gari lao, wakaondoka. Moyoni nilijisikia mtu mwenye bahati sana kwa kujikuta nimepata marafiki wa hali hii katika muda mfupi namna hii. Lakini ni lazima utambue Willy ni mtu mwenye bahati siku zote. Hii ndiyo inayoitwa bahati ya kuzaliwa; na ndio Mama Willy alinitoa nayo tumboni (uk. 28-29).

Mtunzi anaendelea kumwonesha Willy Gamba kama mhusika wa kisangwini kupitia tabia ya kusaka, kutengeneza na kulinda urafiki. Anatuonesha hayo katika matukio yafuatayo yaliyounganishwa:

> Si kawaida yangu mimi Willy kubembeleza sana msichana, hasa akiwa msichana mwenye msimamo kama huyu. Kwani kwa kufanya hivyo unaweza ukaleta kutoelewana naye bure. Ingawaje roho yangu ilikuwa inang'wenya nilijikaza… Niliona hakuna njia zaidi ila kumwacha aende. Nilijua katika siku zilizokuwa zinakuja urafiki wetu ungekuwa wa kukata na shoka, miye Willy nawajulia sana binadamu hawa… Nilimsindikiza mpaka kwenye gari lake. Tulipofika tukaegemea kwenye gari kisha tukasimama tumeangaliana mara nikastukia amepitisha mikono yake juu ya shingo yangu. Midomo yetu ikakutana ulimi wake wa moto ulipenyeza mdomoni mwangu na mara tukawa tumeingia katika ulimwengu wa peke yetu (uk. 29).

Masangwini husaka marafiki na kufanya kila mbinu kuulinda urafiki huo ili faraka isitokee kama ambavyo Willy Gamba anafanya katika matukio yaliyounganishwa hapo juu.

Usangwini unaoneshwa tena kupitia uwazi. Katika tukio lifuatalo, Willy Gamba ambaye ni msondani, anatujuza hivi:

> Nambari moja, ndivyo nilivyokuwa najulikana kikazi. Katika kazi yetu sisi hutumia namba, mimi nilikuwa nambari moja; hivyo, unaweza mwenyewe kuchekecha ukajua kwa nini. Mimi Willy si mtu wa majivuno.

> Watu wengi, hasa wakubwa wa serikali, walinijua tu kwa hii namba yangu. Wengi walikuwa hawajui namba moja ni Willy Gamba, ila kwa watu wachache sana (uk. 35).

Katikati ya tukio hili, mhusika anasema: "...Willy si mtu wa majivuno." Kwa maoni yetu, kauli hii inaonekana kuleta maana iliyo kinyume, hasa inapohusishwa na maelezo ya tukio zima. Hii ni kwa sababu, maana ya jumla ya maelezo ya tukio hili imo katika kumkweza Willy Gamba; lakini amesema hivyo kwa kuwa msangwini si mtu wa kujikweza (hupenda kuonekana mtu wa kawaida miongoni mwa watu). Tumedondoa katika sehemu zilizotangulia za makala hii kuwa ujikwezaji au ujichomozaji ni mojawapo ya sifa za wanadamu wenye haiba ya kikoleriki. Kwa hiyo, kitendo cha Willy Gamba kuukwepa ujikwezaji ni ithibati ya usangwini wake.

Usangwini katika uhusika wa Willy Gamba tunaoneshwa pia kupitia kujiamini kwake mbele ya wakubwa wake wa kazi. Mtunzi anampa Willy Gamba ujasiri wa kusema haya mbele ya bosi wake, Chifu:

> Sasa Chifu ni lazima tuelewane, hili jukumu umenipa mimi. Na inabidi mimi mwenyewe nipange ninavyoona jinsi nitakavyoweza kulitatua tatizo hili, na kama sasa hatuwezi kukubaliana, sijui hii shughuli itatekelezwaje? (uk. 44).

Tukio hili ni kipande cha mazungumzo kati ya Willy Gamba na Chifu kuhusu kuwaruhusu waandishi wa habari kutoka nchi za nje kuingia nchini kwa ajili ya kuandika habari za upotevu wa silaha za wanamapinduzi. Ifahamike kuwa uhusiano wa wahusika hawa wawili (Willy Gamba na Chifu) una misingi ya kijeshi. Hivyo, unapaswa kutawaliwa na dhana ya amri na nidhamu (mdogo anapaswa kutii na kutekeleza linalotoka kwa mkubwa). Hata hivyo, hapa tunaona Willy Gamba anajenga hoja yake kwa jinsi inayochepuka kutoka kwenye misingi ya nidhamu ya kijeshi. Maoni yetu ni kuwa, ujasiri huu wa Willy Gamba unatokana na jinsi alivyojengwa na sifa za kisangwini. Ni usangwini huu ambao baadaye unamfanya Chifu akubaliane na 'ulazima' alioujenga Willy Gamba katika hoja tuliyoidondoa (uk. 45). Kadiri msomaji anavyoendelea kusoma riwaya hii, anakuja kubaini umuhimu wa hoja hiyo inayolazimishwa na Willy Gamba. Waandishi hawa aliolazimisha waingie nchini walitoa mchango mkubwa katika kufanikisha kufichua silaha zilizoibiwa. Hii yote ni tija iliyotokana na usangwini wa Willy Gamba; kwani, yumkini, asingefanikiwa kirahisi katika uchunguzi wake kama asingethubutu kumlazimisha Chifu.

Zaidi, mtunzi anatuonesha moyo wa kuthubutu alionao mhusika wake mkuu. Masangwini wengi huwa na mioyo yenye uthubutu na kujitoa mhanga kama anavyosawiriwa nao Willy Gamba. Haya tunaoneshwa kupitia maongezi yafuatayo:

> "…mimi mwenyewe nilikubali kazi hii, sasa siwezi kurudi nyuma. Vilevile, kwa sababu tukio hili linahusu wapigania uhuru, nipo tayari kwa

> lolote. Wewe mwenyewe unajua moyo wangu ulivyo juu ya ndugu zetu wanaoteswa huko Kusini mwa Afrika…"
> "Naelewa Willy, naelewa sana roho yako ilivyo juu ya ukombozi wa Afrika Kusini. Vijana wote wa Kiafrika wangekuwa na roho kama yako, sasa hivi kungekuwa hakuna ukoloni Afrika" (uk. 46).

Zaidi ya kuthubutu na kujitoa mhanga, Willy Gamba katika matukio haya anaongezewa sifa nyingine ya upendo na huruma kwa watu wa Kusini mwa Afrika. Hizi zote ni sifa wanazokuwa nazo masangwini.

Wepesi wa akili unaotokana na kuwa na kiwango kikubwa cha hisa ya akili unajitokeza katika tukio lifuatalo:

> Nilipokuwa ninapita karibu na nyumba yangu, mara akili ikanijia kuwa afadhali nichukue bastola yangu, kwani nisingeweza kuamini tu kuwa hali itakuwa ya usalama. Nilirudi nyumbani kwangu, nikachukua bastola moja aina ya *38mm* ya kipolisi… (uk. 52).

Huu ni mwanzo tu wa matukio mengi yaliyomo katika riwaya hii yakionesha jinsi akili ya Willy Gamba ilivyo nyepesi kufikiri na kuamua kulingana na mazingira yalivyokuwa. Mtunzi anaukoleza wepesi huo wa akili ya Willy Gamba kupitia maneno ya makomredi wenzake, Sherriff na Veronika. Wanasema:

> …Zaidi ya yote, anaaminika kuwa amehitimu mafunzo ya kikomandoo. Kompyuta ilizidi kuonyesha kuwa Willy Gamba ana I.Q ya hali ya juu sana, hivi ni mtu anayejua kusokoroa matatizo yaliyojisokota sana. Na iliendelea kuonyesha kuwa ameifanyia 'OAU' kazi nzuri sana, hasa kuhusiana na Ukombozi wa Afrika Kusini… Sasa naamini ukiambiwa mtu ana I.Q ya hali ya juu, lazima utambue kuwa kwa kila jambo unalotaka kulifanya yeye yuko hatua nyingi mbele yako (uk. 56, 57).

Hii ni miongoni mwa sifa alizosawiriwa nazo Willy Gamba ikisimama kama mhimili wa kufanikiwa katika kazi yake ya upelelezi.

Umuhimu wa watu wenye hisa ya akili yenye wastani mzuri katika kazi ya upelelezi unaoneshwa tena pale mtunzi anapotongoa sifa za Willy Gamba na namna anavyosaidia kuwajenga kikazi wahusika wasaidizi wanaomzunguka. Kuhusu swali kwamba, 'Je, wasaidizi hawa nao walikuwa na hisa kubwa ya akili?' Mtunzi, kupitia kinywa cha Willy Gamba, anasema:

> Kwa sababu namba mbili, tatu na nne walikuwa safarini huko Kusini mwa Afrika kwa shughuli maalum, ilibidi katika shughuli hii nishirikiane na kijana Eddy Kisanga ambaye alikuwa amejitokeza kuwa kijana shupavu sana katika kazi yetu hii. Eddy alikuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini na mitatu lakini alikuwa na akili ya kuweza kumiliki matatizo na kujifunza mambo magumu katika kazi yetu hii kwa haraka sana. Kitu cha kufurahisha ni kwamba alikuwa mwanafunzi wangu mimi mwenyewe. Hivyo, matendo yake kikazi yalifanana na yangu kiasi kuwa hapa ofisini aliitwa Willy mtoto, na yeye alikuwa akifurahi sana kuitwa hivyo. Kwa hivyo, nilipopeleka jina lake kwenye kamati ya upelelezi nikiwa

> nimeweka sifa zake kama mimi nilivyokuwa nimemwona, haikuwa ajabu kukuta amethibitishwa. Baada ya kuthibitishwa, ilibidi apewe kazi maalum ili kumpima na kuweza kumpa namba. Hivyo, yeye na Sammy Rashidi (namba mbili) walitumwa kwenye kazi maalum huko mjini Johannesburg, Afrika ya Kusini. Kazi hiyo ilitekelezwa vizuri sana. Waliporudi, namba mbili alitoa ripoti juu ya kazi hiyo na ikaonekana sehemu aliyoifanya Eddy ilimshangaza hata Chifu. Eddy alipewa namba ya juu kuliko wote tulivyotegemea kutokana na muda wake kazini. Kutoka kwenye kamati ya usalama alipewa namba 'TANO' (uk. 53).

Mafanikio yanayoelezwa hapa ni ithibati ya kuwa wasaidizi hawa wa Willy Gamba nao walikuwa na hisa ya akili ya kiwango kikubwa. Zaidi, tukio hili linatuongezea sifa nyingine ya usangwini wa Willy Gamba. Sifa hiyo ni utayari wa kutoa ujuzi (*coaching*) kwa watu wanaomzunguka au wanaofanya naye kazi bila kinyongo wala wivu. Katika utendaji au uendeshaji wa ofisi za asasi mbalimbali, hali hii ya wazoefu kuwapa ujuzi walio chini, huchochea ufanisi katika kazi na husaidia kuikuza asasi husika. Ukweli huu unasawiriwa vema katika tukio lililodondolewa hapo juu; ambapo, vijana wa Willy Gamba wanaonekana kutoa msaada mkubwa katika kufikia lengo la upelelezi.

Katika tukio linalofuata, mtunzi anatuonesha jinsi muunganiko wa hisa za akili za watu hawa wawili, Willy Gamba na Eddy Kisanga (mwalimu na mwanafunzi, mtawalia), ulivyotoa matokeo chanya kwa namna ya kushangaza. Hapa, Willy Gamba anamwelekeza mwanafunzi wake mpango-kazi katika namna inayoonesha urafiki:

> Kwa hiyo Eddy, ninachotaka wewe ufanye, kwanza, nataka ukodishe magari manne kutoka kwenye kampuni mbalimbali zinazokodisha magari hapa mjini kama vile *Co-cabs*, *Safari Tours Afrika Ltd*, *Takim's Agencies*, n.k. Gari moja kati ya haya liegeshe kwenye maegesho ya Kilimanjaro Hotel na lingine liegeshe kwenye maegesho ya New Afrika Hotel. Magari mawili yatakayobaki nataka wewe pamoja na kijana mwingine kati yetu mtufuate kila mahali tutakapokwenda leo. Lakini mtufuate kwa siri kabisa kiasi kwamba mtu yeyote asitambue kama mnatufuata sisi… Magari yale utakayoyaegesha Kilimanjaro Hotel na New Afrika Hotel weka swichi ya magari haya chini ya zulia kwa upande anaotoka dereva (uk. 54).

Mpango-kazi huu ulisaidia sana, kwani uliwaokoa katika hatari ya kuuawa katika visa zaidi ya viwili. Hii ni kwa sababu ulisukwa kiakili na mwalimu (Willy Gamba) na kutekelezwa kwa kutumia akili na wanafunzi (Eddy Kisanga na mwenzake). Hapa chini Willy Gamba anajisifu kuhusiana na mpango-kazi huu:

> Nilijaribu nilivyoweza kuangalia kama ninaweza kumwona Eddy na mwenzake lakini wapi. Hakika, vijana walikuwa wanafanya kazi nzuri sana, maana kama mimi Willy sikuweza kuwatambua basi hakuna mtu mwingine tena. Si kama najisifu, ila huo ndio ukweli; mtu akitaka kunitafuta mimi basi ajiweke sawa la sivyo... shauri lake (uk. 66).

Hatimaye, mwalimu ametoa daraja zuri la ufaulu kwa wanafunzi wake (Eddy Kisanga na mwenzake). Ili kuonesha kuwa kweli Eddy alikuwa anafuata vyema nyayo za mwalimu wake katika matumizi ya akili na mbinu katika kazi hii, mtunzi anatuonesha jinsi Willy Gamba mwenyewe alivyo fundi katika mchezo huu. Anatumbia hivi kuhusu namna alivyowachenga maadui wake:

> Kwenye mtaa huu wa Nkrumah niliwakaribia kabisa, nikiwa nimeacha magari mawili tu kati yangu na wao. Niliona mmoja katika gari lao akitoa kichwa nje na kuangalia nyuma, nadhani walikuwa wanadhani nitawafuata na gari langu ambalo wanalijua sana. Lakini hawajui Willy ni mtu wa namna gani… (uk. 82).

Mtunzi anaendelea kudhihirisha usangwini wa mhusika mkuu wa riwaya hii pale anapomuonesha akiwa na marafiki takribani katika kila ofisi kubwa au muhimu. Anatuthibitishia haya katika matukio yafuatayo:

> Jones Mantare alikuwa ananifahamu, maana nilikuwa nimehakikisha kuwa nafahamiana karibu na kila mtu katika ofisi hii ya kamati. Yeye alikuwa akinifahamu kama mfanyabiashara maana ndiyo nilivyojulishwa kwake. Na tokea hapo tulikuwa tunaonana mara kwa mara kwenye sehemu za starehe na kujenga uelewano wa kutosha (uk. 67)… Nimekuwa sina adui Tanzania, hivyo nimekuwa nikiamini kuwa hakuna mtu wa kunifanyia ubaya, maana hata sijawahi kugombana na mtu hapa Dar es Salaam (uk. 96)… Cecil Chimalamo (kiongozi mkubwa wa Chama cha PLF) nilikuwa namfahamu kwa sura, vilevile mambo yake… (uk. 104) (ufafanuzi wa kwenye mabano ni wetu).

Kama tulivyokwishadokeza katika sehemu inayohusu sifa za watu wenye kionjo hiki cha haiba, inatudhihirikia wazi kuwa, kutokana na hulka hii Willy Gamba ni mhusika sangwini.

Sehemu kubwa ya matukio katika riwaya hii inahusiana na jinsi Willy Gamba alivyo na akili nyepesi ya kubashiri, kumaizi na kutatua matatizo. Baadhi ya matukio yanayoonesha uwezo wa Willy Gamba kubashiri hali ya hatari ni:

> Nikasikia kengele ya tahadhari inalia kichwani kwangu, wote watano tulitazamana (uk. 69)… Basi, moja kwa moja wote tulifululiza kwenda kwenye *lift* ya kutupeleka ghorofa ya kwanza ilipo Bandari Grill. Mbele yangu nilimwona Eddy anavuka sehemu ya mapokezi, halafu akazungusha kichwa akaingia kwenye choo kilichopo hapa chini. Hii ilikuwa ishara kuwa alitaka kuniona (uk. 71)… Tulitoka ndani ya gari, Magret akatangulia na kubisha hodi, lakini hakupata jibu. Nilisikia moyo wangu unapiga haraka haraka; hii ni silika niliyozaliwa nayo, na ilikuwa ni ishara kuwa kuna hatari (uk. 73)…Sura ya Sikazwe ilionyesha mshtuko ambao mtu kama mimi tu ambaye angeweza kuuona (uk. 116).

Vipande vyote hivi vya matukio vinadokeza ama lugha-uso au ishara-mwili. Kwa hakika, akili-bwete huwa haina uwezo wa kutafsiri lugha-uso pamoja na ishara za

mabadiliko ya mwili (kama vile moyo kupiga harahaharaka na mwili kusisimka) ili kung'amua nini kitafuatia punde. Bali, huhitaji akili razini inayofanya kazi kwa haraka na kwa usahihi, kama ilivyosawiriwa akili ya mhusika sangwini (Willy Gamba), ili iwe na uwezo huu. Matukio mengine yanayoisawiri sifa hii ya wepesi wa akili yanamwonesha Willy Gamba akiunganisha vipande vidogovidogo vya habari ili kupata jambo lenye maana. Mtunzi anatuonesha hili katika ukurasa wa 70 asemapo: "... basi hapo ndipo huwa naanza kujumlisha moja kwa moja na kupata mbili..." Vilevile, katika ukurasa wa 73 anaongezea, "Sasa nilianza kuongeza hesabu kwamba mbili na mbili na kupata nne..." Matokeo ya tabia hiyo ya uunganishaji wa vipande ilileta matokeo makubwa na ya haraka katika ugunduzi wa silaha zilizopotea.

Licha ya sifa ya kuwa na akili nyepesi, riwaya hii pia ina matukio mengi yanayohusisha sifa ya kujiamini. Zote hizi ni sifa za masangwini. Miongoni mwazo ni:

> Ukuta wa ua huu ulikuwa na urefu usiozidi futi kumi na mbili, hivyo kwangu ukuta kama huu kupanda ni kazi ndogo. Nilikwenda kwenye upande wa lango kubwa, nikazunguka pembe ya kushoto ya ua huu… Mimi nikiwa na silaha ya namna ile hata likija jeshi la watu mia hawaniwezi (uk. 83).
> Shomvu alikuja akikimbia, nikamfungulia mlango na kurudisha mara moja. Aliponiangalia akatambua mimi si Luis alitaka kupiga kelele lakini nilimwahi karate ya kati kati ya kichwa akafa bila kelele (uk. 84)
>
> Kabla sijasema lolote alinambia "Kata kushoto ingia Independence Avenue, halafu ukifika "*Clock Tower*" ingia mtaa wa Railway, halafu shika barabara inayopita kwenye kituo cha polisi usalama barabarani, halafu ukifika kwenye mzunguko ingia kushoto fuata barabara ya Kilwa mpaka nitakapokuelekeza tena. Nasema tena, ujanja wowote utakutokea puani."
> "Usiwe na wasiwasi," nilijibu kiume.
> "Nyamaza," alijibu kwa sauti ya ukali (uk. 90).
>
> "Simama," alisema Lukas.
> Sikusimama. Basi walinijia wote pale kitini kama faru, na mimi Willy tayari nilikuwa nawashwa kumwonyesha huyu mkubwa wao kuwa Willy hasukumwi ovyo… Kama umeme, nilisimama upesi na kukwepa ngumi ya Lukas na kwa sababu alikuwa ameitupa kwa nguvu sana alipepesuka, mimi nikampiga teke kwenye mapumbu akalia kama nguruwe… (uk. 93).

Masangwini huwa hawaogopi kirahisi, hujiamini kufanya jambo lolote hata kama lina kiasi kikubwa cha hatari. Hali hii tunaiona katika matukio haya manne yanayomhusu Willy Gamba (uk. 83, 84, 90 na 93). Willy Gamba anaoneshwa akiwa imara hata pale anapotekwa na kuzungukwa na maadui. Hakati tamaa ya kujiokoa hata anapoona amezungukwa na maadui wengi wenye silaha kali za

kivita. Hiki ni kiwango kikubwa cha kujiamini. Aghalabu, kiwango kama hiki hushuhudiwa kwa watu wenye kionjo cha kihaiba cha usangwini.

**6.0 Hitimisho**

Makala hii imetoa ufafanuzi wa jinsi kionjo cha kihaiba alichosawiriwa nacho mhusika Willy Gamba kilivyoendana na kufanikisha uhusika wake katika riwaya ya *Njama*. Sifa za watu wenye kionjo hiki cha kihaiba ambazo tumezidondoa katika sehemu zilizotangulia zinawiana kwa kiasi kikubwa na sifa alizochorwa nazo Willy Gamba ambazo zimemwezesha kufanikisha majukumu aliyotwishwa katika riwaya hii. Kwa maoni yetu, uwiano huo umemsaidia mwandishi kuwasilisha maudhui yake kwa mrengo wa fasihi pendwa aliouegemea kwa kutumia sifa hizo za kisangwini. Zaidi ya hilo, uwiano huo ni kichocheo kikubwa kinachoifanya riwaya hii na nyinginezo zilizozingatia kaida hii kuwa na unusura (yaani, kubaki katika daraja la juu la kupendwa na watu wa umri na kada mbalimbali kwa muda mrefu). Hivyo, tunahitimisha kwa kuweka msisitizo kuwa ni muhimu sana kwa watunzi kuwianisha majukumu ya mhusika katika kazi za fasihi na vionjo fulani vya kihaiba vya kibinadamu. Hii hurahisisha uelewekaji, utengenezaji wa uhalisi katika akili ya hadhira, uwasilishaji wa ujumbe wenye dhana ya mabadiliko ya kitabia kwa jamii pamoja na kujenga 'utamu' wa kazi husika.

Katika sehemu ya utangulizi tumedokeza vigezo mbalimbali vya kuainisha wahusika wa kazi za kibunilizi. Baada ya maelezo yote ya makala hii, inajuzu kusema kuwa makala hii imeongeza kigezo kingine cha vionjo vya kihaiba kinachoweza kutumika kuainisha wahusika. Kwa kutumia kigezo hiki, wahusika wanaweza kuwekwa katika makundi manne yafuatayo: wahusika wa kiflegmatiki, wahusika wa kikoleriki, wahusika wa kimelankoliki, na wahusika wa kisangwini.

**Marejeleo**


Aras, G. (2015). Personality and Individual Differences: Literature in Psychology - Psychology in Literature, *Procedia - Social and Behavioral Sciences*, 185: 250-257.

Bobgan, M. & Bobgan, D. (1992). "Christians and the Four Temperaments Theory," in http://www.psychoheresy-aware.org/images/4temp_01.pdf. Accessed on 21 August 2018.

Ekstrand, D.W. (ht). "The Four Human Temperaments," in *www.thetransformedsoul.com/.../the-four-human-temperaments*. Accessed on 19 August 2018.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Mture Educational Publishers Ltd.

Media Sportlight (1994). "A Biblical Analysis of Religious and Secular Media: Special Report on Four Temperaments, Astrology and Personality

Testing," in www.mediasportlight.org/pdf/FOURTEPERAMENTS.PDF. Accessed on 19 August 2018.

Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1995). *Historia na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: *Kozi za Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Musiba, A.E. (1981). *Njama*. Dar es Salaam: Continental Publishers

Njogu, K. na Chimerah, R. (2011). *Ensaiklopidia ya Ufundishaji wa Fasihi: Ufundishaji wa Fasihi – Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Okal, B.O., Ambuyo, B. A. & Amukowa, D. N. (2012). The Functionality of Four Temperaments and Communication Theories towards the Realisation of Peaceful General Elections in Kenya, *Journal of Sociological Research*, 3(1): 55 - 66.

Septiana, R.S. (2017). Personality Development in Hiccup in Cressida Cowell's *How to Train your Dragon*. Thesis Submitted for Degree in English Language Education. Sanata Pharma University.